JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA KUHUSU HUDUMA ZITOLEWAZO BRELA (FAQs).

NENO LA AFISA MTENDAJI MKUU

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imeandaa kitabu hiki kwa ajili ya kuJibu maswali ambayo mara kwa mara yamekuwa yakiulizwa na wadau wetu. Lengo likiwa kuongeza uelewa wa wateja wetu kuhusu huduma tunazotoa na kuwawezesha kuzifikia huduma zetu kwa urahisi wakiwa popote.

Ahadi yetu kwa Wadau wetu siku zote ni kuwapatia huduma bora na kwa wakati, kitabu hiki ni sehemu ya jitihada za kutengeneza mazingira rafiki kwa wadau wetu ili waweze kupata hudum kwa urahisi na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu zilizopo.

Ndani ya kitabu hiki Wadau wetu watapata majibu kwa maswali yote ambayo yamekuwa yakiulizwa kuhusu vigezo na taratibu za kufanya Sajili za kibiashara, kupata Usajili au Leseni ya Kiwanda pamoja na huduma za baada ya Sajili au kupata Leseni ili yawe mwongozo kwa wadau wetu katika kupata huduma yoyote wanayohitaji.

BRELA itaendelea kupokea maoni na mapendekezo ya kuboresha kitabu hiki kutoka kwa wadau mbalimbali ili kuweza kufikia kiwango cha matarajio yao na kuweza kutoa majibu ambayo yataweza kuwasaidia katika kuandaa maombi yao kwa njia ya mtandao na kuweza kuwasilisha kwa wakati.

Ni Imani yangu kwamba kwa kupitia kitabu hiki malalamiko kuhusu changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikijitokeza wakati wa kuandaa na kutuma maombi ya huduma mbalimbali yatapungua na kuwa chachu ya Wadau wengi zaidi kupata huduma za BRELA.

DIBAJI

Wakala wa Usajili Wa Biashara na Leseni (BRELA) ilianzishwa chini ya Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya mwaka 1997 na kuzinduliwa rasmi tarehe 03 Disemba , 1999 chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Jukumu la msingi ni kusimamia shughuli za kibiashara nchini kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo kwa lengo la kuweka mazingira mazuri ya kibiashara.

Uwekaji wa mazingira mazuri ya kibiashara pia unahusisha upatikanaji wa taarifa muhimu kwa wadau kuhusu huduma zinazotolewa. Ndani ya kitabu hiki kuna majibu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara kuhusu huduma zinazotolewa na BRELA, ambayo yatawezesha kuwa na uelewa kuhusu huduma inayohitajika na namna ya kupata huduma hiyo.

Kitabu hiki kimegawanyika katika sehemu nne, ambazo zina maswali na majibu kuhusu Usajili wa Kampuni, Majina ya Biashara, Milifi Bunifu ambayo imegawanyika katika maeneo mawili ya Usajili wa Alama za Biashara, Huduma na kutapa Hataza. Sehemu ya mwisho ni huduma za Leseni ambayo imegawanyika katika sehemu mbili yaani, Leseni za Biashara Kundi “A” na Leseni za Viwanda.

SEHEMU YA KWANZA

MASWALI NA MAJIBU KUHUSU HUDUMA ZA KAMPUNI

A. IDARA YA KAMPUNI

I. USAJILI WA KAMPUNI

1. Je ni mambo gani muhimu ya kuzingatia ili kuanza hatua za usajili wa Kampuni?

Ili kuanza hatua za usajili wa Kampuni wahusika wanatakiwa kuwa na vitu vifuatavyo:-

Namba ya Kitambulisho cha Taifa inayotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kwa watanzania, na nakala ya hati ya kusafiria kwa raia wa kigeni.

(b) Barua pepe kwa wahusika wote (email addresses)
(c) Namba za simu za kiganjani za wahusika
(d) Jina la Kampuni
(e) Anuani ya makazi / Ofisi
(f) Katiba ya kampuni (Memorandum and Articles of Association

2. Ni njia gani inayotumika kufanya sajili mbalimbali BRELA?

Usajili unafanyika kwa njia ya mtandao kupitia Mfumo wa Usajili unaoitwa Online Registration System (ORS).

Wakati wa kufanya Usajili wahusika wahakikishe wanakuwa na vitu vifuatavyo:-

- Namba ya Kitambulisho cha Taifa inayotolewa na NIDA kwa watanzania au Hati ya Kusafiria kwa raia wa kigeni.
- Barua pepe kwa wahusika wote (email addresses) na taarifa za anuani za, makazi kwa wahusika na za ofisi.
- Namba za simu za kiganjani za wahusika (wanahisa na wakurugenzi).

- Jina la Kampuni linalopendekezwa
- Katiba ya Kampuni (Memorandum and Articles of Association).

Kwa msaada zaidi wakati wa kufanya usajili wasiliana nasi kwa barua pepe usajili@brela.go.tz au simu Kituo cha Miito namba 0222 212 800

3. Je kuna aina ngapi za kampuni?

Kuna aina nne za Kampuni.

(i) Kampuni binafsi
(ii) Kampuni za umma
(iii) Kampuni za kigeni
(iv) Kampuni za Serikali

4. Hatua zipi za kufuata ili kukamilisha usajili wa kampuni kwa njia ya Mtandao (ORS)?

1. Tembelea mfumo wa usajili kupitia https://ors .brela.go.tz au kupitia tovuti ya BRELA www.brela.go.tz na bofya LIMITED COMPANY ONLINE REGISTRATION.
2. Kama huna akaunti kwenye mfumo, bofya “huduma mtandao kwa watumiaji wasiosajiliwa, Ingia kwenye mfumo kwa kuweka jina la mtumiaji na neno la siri (nywila).
3. Bofya “anza”kisha chagua “huduma mtandao”.
4. Chagua kampuni
5. Kwenye aina ya huduma chagua Usajili wa kampuni mpya , kisha bofya endelea.
6. Kwenye aina ya kampuni chagua aina ya kampuni Mfano “Kampuni ya faragha imepunguzwa kwa hisa ; kisha bofya Endelea.
7. Kwenye fomu ya maombi, jaza taarifa zote zinazotakiwa ambazo zimeweka alama ya nyota nyekundu(*)
8. Kumbuka kubofya kitufe cha Hifadhi kwa kila taarifa unayoingiza zisipotee.
9. Sehemu ya Mwombaji Jaza Kauli ya uwakilishi kama ni Mkurugenzi/ Katibu/Mwakilishi

10. Kama mwombaji anaweza kubadili taarifa kwenye mfumo wa ORS, bofya" anaweza kurekebisha taarifa ORS".
11. Sehemu ya kitambulisho jaza tarehe ya uhasibu na jina la kampuni. Kama uliomba kuhifadhi jina jaza namba ya kuhifadhi.
12. Jaza taarifa zote kwenye sehemu ya ofisi ya kusajiliwa.
13. Kwenye sehemu ya shughuli ya kibiashara, bofya Ongeza; kisha jaza taarifa za wakurugenzi wa kampuni. Angalu wawili.
14. Sehemu ya Wakurugenzi, bofya Ongeza, kisha jaza taarifa za wakurugenzi wa kampuni. Angalau wawili.
15. Sehemu ya Katibu wa Kampuni, jaza taarifa za katibu wa Kampuni.
16. Sehemu ya Mtaji wa Kampuni , chagua aina ya mtaji wa kampuni kama ni Kawaida au Mwingine.
17. Sehemu ya Hisa za mtaji zilizotolewa, weka Idadi ya Hisa zilizotolewa na thamani ya kila hisa.
18. Sehemu ya Wana hisa bofya Ongeza na ingiza taarifa za wanahisa wasiopunga wawili.
19. Sehemu ya idadi ya hisa zilizoshikiliwa; chagua mwana hisa kutoka kwenye orodha sehemu ya "chagua mwanahisa kutoka orodha na Daraja kisha Bonyeza Add shareholders to the table below
20. Sehemu ya wawakilishi, weka taarifa za wawakilishi (Watu wanaoweza kufanya marekebisho au mabadiliko kwenye mfumo wa (ORS). Kama Wakurugenzi / wanahisa wanaweza kufanya marekebisho, bofya "Anaweza kurekebisha taarifa kwenye ORS , kisha bonyeza kitufe cha Endelea.
21. Mfumo utakupeleka sehemu ya kupakua na kupakia fomu na malengo na katiba ya kampuni. Subiri Consolidated form kisha ipakue, saini weka tarehe na scan fomu hiyo.
22. Pakua fomu ya maadili, saini na gonga muhuri wa kampuni.
23. Pakia consolidated form, fomu ya maadili (Integrity form), malengo ya katiba ya kampuni (Memorandum and Articles of Association), kisha bofya "Endelea"
24. Mfumo utakupeleka kwenye ukurasa wa kufanya malipo, Chagua aina ya njia unayotaka kufanya malipo.
25. Pakua taarifa ya maelekezo ya namna ya kufanya malipo na kisha fuata maelezo.

26. Baada ya kufanya malipo maombi yako yatatumwa na mfumo kwa ajili ya kufanyiwa kazi BRELA na yatahama kutoka sehemu ya Orodha yangu kwenda sehemu ya Maombi.

5. Ni viambatisho gani ambavyo vitahitajika kwa ajili ya kukamilisha usajili wa kampuni?

(i) Katiba ya Kampuni,
(ii) Fomu namba 14a (Consolidated form),
(iii) Fomu ya maadili,
(iv) Nakala ya hati ya kusafiria kwa wasio raia wa Tanzania na nyaraka nyingine ambazo msajili ana mamlaka ya kuziomba anapo ona inafaa.

6. Je usajili wa kampuni unagharimu kiasi gani?

Ada ya usajili wa Kampuni inategemea na mtaji wa Kampuni kama ilivyoandikwa katika Katiba ya Kampuni kama ifuatavyo:-

1. Mtaji unaozidi TZS.20,000/= na usiozidi TZS. 1,000,000/= ada ni TZS 95,000 /=
2. Mtaji unaozidi TZS. 1,000,000/= na usiozidi TZS. 5,000,000/= ada ni TZS. 175,000 /=
3. Mtaji unaozidi TZS. 5,000,000/= na usiozidi TZS. 20,000,000/= ada ni TZS. 260,000/=
4. Mtaji unaozidi TZS. 20,000,000/= na usiozidi TZS. 50,000,000/= ada ni TZS. 290,000 /=
5. Mtaji unaozidi TZS. 50,000,000/= ada ni TZS. 440,000 /=

7. Nawezaje kulipa ada ya usajili wa Kampuni baada ya kuingiza taarifa katika mfuno wa ORS?

Baada ya kukamilika ujazwaji wa taarifa katika mfumo, utatengeneza namba ya malipo kupitia Mfumo wa Malipo ya Serikali (GePG). Baada ya kupata namba ya malipo unaweza kufanya malipo kupitia mitandao ya simu au benki.

8. Baada ya kujaza taarifa kwa ajili ya usajili wa Kampunni na kufanya malipo huchukua muda gani ili maombi kukamilika na kupata cheti?

Endapo taarifa zilizoingizwa katika mfumo zitakuwa sahihi kwa mujibu wa sheria, cheti hutolewa kwa njia ya mfumo ndani ya siku tatu na ikiwa taarifa za ziada zitahitajika pia ndani ya siku tatu atakua amejulishwa ili kufanya marekebisho au nyongeza .

9. Je ni namna gani naweza kupata cheti cha usajili wa Kampuni>

Baada ya maombi kupitishwa na msajili, cheti cha usajili hutolewa kupitia mfumo wa ORS katika akaunti iliyotumika kuwasilisha maombi ya usajili sehemu ya maombi (application)

10. Je kampuni hufanya malipo ya kuwasilisha taarifa ya mwaka kila baada ya muda gani?

Kila baada ya miezi 12 baada ya kampuni kusajiliwa

11. Nini hutokea pindi kampuni inapochelewa kuwasilisha taarifa ya mwaka kwa wakati?

Kampuni ikichelewa kuwasilisha taarifa ya mwaka kwa wakati italazimika kulipa ada ya kuchelewa kuwasilisha ya Shilingi 2,500/= kwa kila siku ilizocheleshwa. Kampuni inapochelewa kuwasilisha taarifa hizi kwa wakati inakuwa katika hatari ya kufutwa na Msajili wa Makampuni kwa mujibu wa sheria.

12. Je hatua zipi za kufuata ili kufanya mabadiliko mbali mbali ya kampuni?

Kuna hatua mbalimbali za kusajili wakati wa kufanya mabadiliko kwenye Kampuni. Mfumo wa ORS unampatia mteja uhuru wa kuchagua

mabadiliko anayotaka kuyafanya kwa kuingiza taarifa za mabadiliko husika.

13. Ninawezaje kuwasilisha taarifa ya mwaka ya kampuni?

Kwa kujaza fomu Na. 128 inayopatikana katika mfuno wa ORS na kuwasilisha kupitia mfumo huo .

14. Ninawezaje Kuhuisha taarifa za kampuni kupitia mfumo wa BRELA ORS?

Kwa kufungua akaunti katika Mfumo wa ORS na kuingiza taarifa za Kampuni zifuatazo:-

i) Jina la Kampuni, anwani ya kampuni.
ii) Namba za Vitambulisho vya Taifa vya Wakurugenzi. na Wanahisa.
iii) Namba za utambulisho wa mlipa kodi.
iv) Anwani ya makazi ya Wakurugenzi na Katibu wa Kampuni.
v) Namba za simu za Wakurugenzi na Wanahisa.
vi) Mtaji wa Kampuni na mgawanyo wa hisa kwa kila mwanahisa, kwa kampuni yenye mtaji.

15. Je ninawezaje kupata taarifa za kampuni iliyosajiliwa?

Kwa kuomba kupitia Mfumo wa ORS au kutembelea Ofisi za BRELA ambapo mteja atalipia Ada ya kupekua jarlada kiasi cha Shilingi 3,000 na atapatiwa jarlada husika ili aweze kupekua moja kwa moja...

16. Je Kampuni inaweza kufungwa kwa utaratibu upi?

Kampuni inaweza kufungwa kwa njia mbili :-

(A) Kwa hiari ya wamiliki wa Kampuni au
(B) Kwa amri ya mahakama.

17. Ni hatua zipi za kufuata ili kufunga Kampuni?

Kampuni inaweza kufungwa kwa njia mbili:-

(a) Kufungwa kwa hiari na wamiliki wa Kampuni
(b) Kwa Amri ya Mahakama

Kampuni inayofungwa kwa hiari ya wamiliki wa Kampuni hufuata hatua zifuatazo:-

i) Kwa kukaa kikao cha wanahisa na kupitisha Azimio la kufunga Kampuni husika.
ii) Kutangaza Azimio katika Gazeti la Serikali na Gazeti la kawaida linalotoka kila siku.
iii) Kupata cheti cha uthibitisho kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)kuwa Kampuni haidaiwi Kodi ya Serikali.
iv) Kuwasilisha taarifa ya mwaka endapo Kampuni haijawasilisha.

18. Je ninawezaje Kuhifadhi Jina la Kampuni?

Kwa kutuma maombi ya jina lililopendekezwa kupitia kwenye mfumo wa ORS na baada ya jina kukubaliwa huweza kuhifadhiwa kwa siku 60 kwa kulipia ada ya uhifadhi wa jina ya TZS. 50,000/=.

MMILIKI MANUFAA WA KAMPUNI

1. Ni nini maana ya Miliki manufaa wa Kampuni (Beneficial Owner) ?
Mmiliki manufaa wa Kampuni ni mtu ambae sio lazima jina lake lionekane kati ka nyaraka za Kampuni lakini anamiliki, anahodhi au anaendesha asilimia kubwa ya Uwekezaji katika kampuni au makubaliano ya kibiashara kwa kupitia mtu mwingine anaeonekana kwenye nyaraka za kampuni.

2. Ni sheria ipi inayoruhusu taarifa za Mmiliki manufaa kutolewa?
Taarifa za mmiliki Manufaa ni taarifa za siri (confidential information) na

hivyo haziwezi kutolewa kwa umma. Hata hivyo Sheria ya Makampuni Sura 212 imempa mamlaka Msajili wa Makampuni kukusanya na kutoa taarifa za Wamiliki Manufaa kwa Taasisi ambazo zimepewa mamlaka ya kisheria kufanya uchunguzi, upelezi, kupambana na makosa ya utakatishaji fedha, ufadhili wa ugaidi na kodi nchini Tanzania.

Ni hatua zipi za kufuata ili kuwasilisha taarifa za Mmiliki Manufaa? Kanuni za Wanufaika wa Mwisho za mwaka 2020 zimeweka utaratibu wa kuwasilishwa kwa taarifa za wanufaika wa mwisho kwa Msajili wa Makampuni ambapo Kamapuni imepewa wajibu wa kukusanya taarifa za wanufaika wa mwisho na kuwasilisha taarifa hizo kwa Msajili wa Makampuni kwa kupitia Fomu na 14b.

Ni kampuni zipi zinatakiwa kuwasilisha taarifa za Mmiliki Manufaa Kampuni zote zinazosajiliwa na zilizokwsiha pata usajili ukiachilia kampuni za nje zilizosajili matawi nchini (foreign companies) zinawajibu wa kisheria kukusanya na kuwasilisha kwa Msajili wa Makampuni taarifa za Wamiliki manufaa waliomo kwenye kampuni zao.

3. Ni lini kampuni inatakiwa kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa? Uwasilishaji wa taarifa za Wamiliki manufaa upo wa aina mbili:-

4. (a) Kampuni ambazo tayari zimesajiliwa zinatakiwa kuwasilisha taarifa za wamiliki manufaa kabla ya tarehe 31 Desemba, 2021.

5. (b) Kampuni mpya zinatakiwa kuwasilisha taarifa zake ndani ya siku 30 tangu tarehe ya kusajiliwa.

6. **Ni viambatanisho gani ambavyo vitahitajika kwa ajili ya kuwasilisha taarifa za Mnufaika wa mwisho?**
   Fomu 14b iliyobeba taarifa za Wanufaika wa Mwisho inaweza kuambatishwa na nyaraka zifuatazo;
   (a) Kiapo cha mmiliki wa hisa/ mwanachama wa kampuni ambaye hamiliki manufaa ya hisa (fomu 14d)

(b) Kiapo cha mmiliki manufaa ya hisa lakini jina lake halionekani katika orodha ya wanachama / wamiliki wa kampuni (fomu namba 14 e)

(c) Endapo mmiliki manufaa ni mwanasiasa maarufu (Pollitically exposed person) kiapo cha mmiliki wa hisa asiye miliki manufaa Kama ni raia wan chi nyingine – Nakala ya pasi ya kusafiria (Passport)

7. Ni nani / taasisi zipi zinaruhusiwa kupata taarifa za Mnufaika wa Mwisho?

Sheria imetaja Taasisi ambazo zinaweza kupewa taarifa za wamiliki wa mwisho. Taasisi hizo ni zile zenye mamlaka ya ya kisheria kufanya uchunguzi, upelezi, kupambana na makosa ya utakatishaji fedha, ufadhili wa ugaidi na kodi nchini Tanzania kama vile;

i. Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa – TAKUKURU
ii. Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu Tanzania – FIU
iii. Mamlaka ya Mapato Tanzania – TRA
iv. Jeshi la Polisi
v. Taasisi za Serikali zinazosimamia uwezeshaji wa wananchi kiuchumi

Ili kuweza kutumia mfumo huu ni lazima watumiaji wazingatie yafuatayo:-

(a) Kuwa na Namba ya Utambulisho wa Utaifa (National Identification Number (NIN) inayotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

(b) Ikiwa unatarajia kuwa Mkurugenzi wa Kampuni (Director) awe na Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN) inayotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

(c) Wakati unaandaa malengo na Katiba ya Kampuni (Memorandum and Articles of Association) hakikkisha malengo unayojiwekea yameendana na shughuli unazozichagua katika mfumo wa ORS kwa mujibu wa madaraja ya ISIC (ISIC Classification) ambayo yanapatikana katika mtandao na katika Tovuti ya BRELA.

SEHEMU YA PILI

MASWALI NA MAJIBU KUHUSU HUDUMA YA USAJILI WA MAJINA YA BIASHARA

1. **Ni taratibu zipi za kufuata ili kusajili Jina la Biashara?**
   Kwanza utatakiwa kufungua Akaunti kwenye mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao kupitia mfumo wa ORS na kuingiza taarifa za Jina la Biashara.

2. **Ni vitu gani ambavyo vinaweza kuniwezesha kumiliki Jina la Biashara?**
   Kwanza unatakiwa kuchagua jina litakalotumika katika biashara yako na kusajili ikiwa jina unalotumia kwenye biashara yako halija fanana/sajiliwa na mtu mwingine basi utasajili na kumiliki jina husika katika biashara yako. Ikiwa jina la biashara limefanana jina lingine lililosajiliwa na linatumika kwa biashara nyingine utatakiwa kubadili jina hilo.

3. **Ni taarifa zipi ambazo zitanilazimu kujaza katika Mfumo wa ORS pindi ninapo sajili Jina la Biashara?**
   Mfanya biashara atatakiwa kujaza taarifa za umiliki kwa kutumia kitambulisho cha Taifa (NIDA) anwani ya Barua Pepe, namba za simu, sanduku la barua, anuani ya eneo la biashara, anuani ya makazi ya biashara na aina ya biashara inayofanywa,

4. **Je ni gharama kiasi gani inahitajika ili kukamilisha usajili wa Jina la Biashara**
   Ada ya Usajili wa Jina la Biashara ni shilingi za kitanzania 20,000/=

5. **Usajili wa Jina la Biashara unachukua muda gani kujibiwa baada ya kuwasilisha maombi?**

   Inachukua muda usiozidi siku mbili ili kupata cheti cha usajili wa Jina la Biashara ikiwa taarifa zilizowasilishwa kwa ajili ya usajili wa Jina la

Biashara zipo sahihi na ikiwa kuna marekebisho ndani ya siku mbili mteja atakuwa amepata taarifa ili kufanya marekebisho husika.

6. **Je nitajuaje kama maombi yangu yameshafanyiwa kazi?**
   Utapata taarifa kupitia anwani ya barua pepe iliyowekwa kipindi taarifa zinaingizwa kwenye mfumo na pia katika akaunti ya mhusika ya ORS.

7. **Ni namna gani nitaweza kupata cheti changu cha usajili wa Jina la Biashara baada ya maombi kukamili?**
   Utapata cheti cha usajili kupitia kwenye akaunti iliyotumika kuingiza taarifa wakati wa usajili wa jina hilo la biashara.

8. **Je ninawezaje kufanya mabadiliko ya Jina la Biashara?**
9. Ikiwa unataka kufanya mabadiliko ya jina la biashara utatakiwa kuingia kwenye mfumo uliotumika kusajilia kwa kuingiza taarifa za mabadiliko husika na kujaza fomu Na.6. **Baada ya kupata cheti cha Jina langu la Biashara ni baada ya muda gani natakiwa kufanya malipo ya utunzaji wa jalada?**

Malipo ya utunzaji wa Jina la Biashara (Maintenance fee) yanafanyika kila mwaka. Ada ya mwaka ni Shilingi 5,000/=.

10. **Je nikichelewa kufanya malipo ya mwaka kwa wakati kuna faini yoyote ambayo nitatozwa siku ambayo nitakuwa nafanya malipo?**

Hakuna faini ya kuchelewa kufanya malipo ya m waka isipokuwa mhusika atatakiwa kulipia miaka yote ambayo hakufanya malipo.

11. **Ni kitu gani naweza kufanya ili nisirudishwe na marekebisho ya mfanano wa Majina?**

Kufanya utafiti kwa kupitia mfumo wa ORS uliowekwa kwa ajili kufanya ukaguzi wa majina kwa kuangalia asilimiia (%) ya mfanano wa majina.

12. Ni mfanano wa asilimia ngapi ambao unashauriwa baada ya kufanya utafiti wa Jina?

Chini ya asimia 50

13. Je ni vitu gani vinavyozingatiwa katika mfanano wa majina ya Biashara?

(a) Kama majina yanafanana neno kwa neno.
(b) Kufanana kwa karibu
(c) Kufanana kwa matamshi mfano skuli na School
(d) Kufanana kwa muonekano
(e) Kufanana kwa tafsiri Kiswahili / Kiingereza

14. Tembelea mfumo wa usajili kupitia https://ors, brela.go.tz au kupitia tovuti ya BRELA www.brela.go.tz na bofya LIMITED COMPANY ONLINE REGISTRATION.

Kupitia mfumo wa ORS baada ya kufanya malipo ambapo unaweza kuomba "standard search" au custom search' au kutembelea ofisi za BRELA na kufanya upekuzi (perusal) wa jalada husika.

15. Ni namna gani ninaweza kubadili Jina la Biashara na kuwa Kampuni?

Unaweza kubadilisha jina la biashara na kuwa Kampuni kwa kuanza na utaratibu wa kulifunga jina la Biashara na kisha kuandaa nyaraka kwa ajili ya usajili wa kampuni kwa kutumia jina lililokuwa linatumika.

16. Je ninawezaje kuhuisha taarifa za Jina la Biashara kupitia mfumo wa ORS?

Unaweza kuhuisha taarifa za jina la biashara kwa kufungua
Akaunti ya ORS na kuingiza taarifa za jina la biashara husika katika mfumo huo. Taarifa hizo ni pamoja na namba ya usajili wa jina la biashara, namba ya kitambulisho cha NIDA kwa wamiliki wa sasa, anuani/

eneo la biashara pamoja na makazi ya mmiliki, anuani ya barua pepe, namba ya simu ya kiganjani, shughuli zinazofanywa/aina ya biashara na majina ya wanaoendesha Akaunti ya Benki.

15. Ninawezaje kufunga jina la biashara?

Kwa kupitia katika Mfumo wa ORS ambapo utatakiwa kujaza fomu namba 7 nakuiwasilisha kupitia mfumo huo na endapo Jina husika la Biashara halijahuishwa katika Mfumo basi fomu namba 7 ikiwa imeambatanishwa na vyeti halisi vitawasilishwa BRELA kwa ajili ya kufutwa katika daftari la Msajili wa Majina ya Biashara. Maombi ya ufungaji wa Jina la Biashara huambatana na malipo ya ada ya ufungaji wa Jina la Biashara.

B. MILIKI UBUNIFU

Nini maana ya Miliki Ubunifu?

Miliki Ubunifu ni nyanja inayohusu uwezo wa ubunifu wa Mtu katika kuunda vitu au kutoa huduma. Ni Mfumo unaotambuliwa chini ya mfumo wa sheria za ulinzi wa bunifu mbalimbali.

I. ALAMA ZA BIASHARA NA HUDUMA

1. Nini maana ya Alama ya Biashara na Huduma?

Ni alama ya kipekee ambayo imebuniwa na mtu kwa madhumuni ya kutofautisha bidhaa anazozitengeneza au huduma anazozitoa na bidhaa au huduma zinazotolewa na watu wengine wanaotengeneza bidhaa au kutoa huduma zinazofanana na za kwake.

Alama ya Biashara au Huduma inaweza kuwa neno, umbo, mchoro, nambari, kifupi cha jina halisi au jina bunifu la mmiliki, kampuni au jina/neno la kubuni isipokuwa yale ambayo yamekatazwa.

2. Ni namna gani ninaweza kusajili Alama ya Biashara au Huduma?

Muombaji anatakiwa kutuma maombi BRELA kwa njia ya mtandao kupitia Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao [Online registration System (ORS)] ambapo atatakiwa kutengeneza Akaunti na kuingiza taarifa za Alama yake.. Ili kutengeneza akaunti kwa Mtanzania analazimika kuwa na namba ya kitambulisho cha NIDA, barua pepe, namba ya simu ya mkononi na kutengeneza nywila (password). Wasio raia wa Tanzania watapaswa kuwasilisha maombi kupitia Mawakala wa Alama za Biashara na Huduma walioko nchini (Trade and Service Mark Agents).

3. Ni vigezo gani ambavyo vinahitajika ili kupata Alama ya Biashara au Huduma?

(i) Alama iwe ya kipekee ambayo ameibuni mmiliki mwenyewe .
(ii) Alama hiyo isifanane na alama ambayo ilishasajiliwa na mtu mwingine katika daraja husika.
(ii) Isielezee sifa ya bidhaa au huduma inayohusu daraja husika.
(iii) Isiwe kinyume cha sheria na maadili.

4. Je kuna tofauti gani katika ya Alama ya Biashara na Alama ya Huduma?

Alama za biashara zinahusisha bidhaa zinazoshikika kama vile nguo, vitabu, machine nk. Alama za huduma zinahusisha huduma ambazo haziwezi kuonekana na hazishikiki kama vile huduma za kifedha, usafirishaji, bima nk. Tofauti nyingine ni kuwa alama za biashara na huduma zinatofautishwa kwa madaraja ambapo Alama za biashara ni kuanzia daraja la 1 - 34 na kwa upande wa huduma ni kuanzia daraja la 35 – 45 la Nice International Classification of Goods of Services.

5. Je huchukua muda gani ili kukamilisha maombi ya Alama za Biashara au Huduma?

Maombi ya usajili wa Alama yakisha kubaliwa na BRELA, yanatangazwa na hutakiwa kukaa katika Jarida la Alama kwa muda wa siku sitini toka

siku ya kutangazwa kwa mujibu wa Sheria, baada ya siku sitini kama hakutakuwa na pingamizi, mwombaji hutakiwa kuwasilisha fomu TM/SM 8 na kulipia ada ya usajili ili kupatiwa cheti cha usajili wa Alama. Hivyo kuanzia kuwasilisha maombi ya usajili wa Alama mpaka kusajiliwa huchukua wastani wa miezi mitatu.

6. Ni jinsi gani naweza kupata cheti changu cha usajili wa Alama ya Biashara au Huduma?

Cheti cha usajili wa Alama ya Biashara/Huduma hupatikana kwa njia ya Mtandao (ors.brela.go.tz) baada ya mwombaji kuwasilisha fomu TM/SM 8 na kulipia ada ya usajili (kwa njia ya mtandao)

7. Ni namna gani naweza kufanya mabadiliko katika Alama ya Biashara au Huduma?

Mabadiliko yoyote ya kabla na baada ya usajili wa alama za biashara na huduma hutakiwa kuwasilishwa kwa Msajili kwa ajili ya kubadilisha kumbukumbu. Mwombaji anafanya mabadiliko kwa kujaza fomu husika zinazopatikana katika mtandao wa BRELA sehemu ya alama za biashara na huduma.

8. Je nitawezaje kupata taarifa kama Alama ya Biashara au Huduma imesajiliwa BRELA?

Taarifa za Alama zinapatikana kwa njia ya mtandao wa ORS. Mwombaji ataingia katika akaunti yake ya ORS halafu atabonyeza batani ilioandikwa “information services” na kuchagua “standard search” au “custom search” na kuandika jina la alama ambayo anataka kufahamu kama imesajiliwa pamoja na daraja lake (class) na kulipia ada ya Shilingi 10,000/=, kisha mwombaji atapata taarifa hiyo kupitia akaunti yake ya ORS moja kwa moja au kutumiwa taarifa hiyo kama alichagua “custom search-tailor made.”

9. Ni sifa zipi zinaweza kuitambulisha Alama ya Biashara au Huduma?

(a) Alama ikubaliane na taratibu za kisheria za usajili wa alama za biashara na huduma
(b) Alama isifanane na alama nyingine ambayo imelindwa na mtu au kampuni nyingine
(c) Iwe rahisi kusomeka kama ni neno na isiwe na maana ambazo hazikubaliki kisheria na kimaadili
(d) Haielezei sifa au ubora wa bidhaa au huduma inazoziwakilisha

10. Muda gani na Ada kiasi gani itahitajika kuhuisha taarifa baada ya usajili wa Alama ya Biashara au Huduma?

Baada ya miaka saba toka tarehe ya usajili wa Alama ya Biashara au Huduma, mmiliki hutakiwa kuhuisha Alama yake kwa kuwasilisha fomu TM/SM 9 na kulipia ada ya Tshs. 30,000/= ya kuhuisha na Tshs. 5,000/= ya kutunza Alama ya Biashara au Huduma husika, baada ya hapo Alama huhuishwa kila baada ya miaka kumi

Ada ya kuchelewa kuhuisha Alama ya Biashara au Huduma ni Tshs. 30,000/= ambayo huwasilishwa kwa kujaza Fomu Namba TM/SM 10 na kuiwasilisha kwa njia ya mtandao wa ORS.

11. Ni kwa namna gani naweza kulipia malipo ya Alama ya Biashara au Huduma baada ya muda wake kuisha?

Mteja atalipia kwa kupitia mfumo wa ORS, ataingia kwenye akaunti yake halafu ataenda upande wa alama za biashara atabofya batani iliyoandikwa filing of other documents alafu atachagua filing type hapo anaweza akafanya malipo anayotaka KWA KUCHAGUA FOMU aliyoijaza kulingana na anachotaka kulipia

12. Baada ya kutuma maombi ya usajili wa Alama ya Biashara au Huduma Je ni hatua zipi hufuata hadi maombi kukamilika?

(a) Kwanza kupitiwa na Afisa wa BRELA kuangalia kama taratibu

na kanuni zimefuatwa (formalitity examination)

(b) Ombi la kupewa namba ya usajili

(c) Ombi la kufanyiwa ukaguzi wa jina au logo kama tayari limesajiliwa BRELA katika hilo daraja (class) ambalo mwombaji anaomba

(d) baada ya hatua hizo tatu kuisha maombi hutumwa kwa mtoa maamuzi (Decision maker)

13. Je? natakiwa kwenda TRA baada ya kupata cheti cha usajili wa Alama ya Biashara au Huduma?

Hapana

14. Ni faida zipi naweza kuzipata baada ya kusajili Alama ya Biashara au Huduma?

(a) Kuwa na haki ya kipekee kutumia alama husika na kuwazuia wengine kutumia alama hiyo isipokuwa kwa ruhusa au ridhaa yako.

(b) Kudhibiti ushindani wa bidhaa au huduma katika soko.

(c) Kuendeleza umaarufu wa ubora wa bidhaa au huduma.

(d) Kuhifadhi ulinzi wa alama iliyosajiliwa pamoja na mabadiliko husika.

(e) Kumpatia mbunifu wa Alama husika kipato kwa njia ya kuuza Alama au kutoa haki ya matumizi kwa mtu mwingine.

(f) Kuwawezesha watumiaji wa bidhaa kutambua na kuchagua alama au huduma kutokana na ubora.

(g) Kumpa mmiliki haki ya kisheria , kumchukulia hatua mtu anayeiga alama hiyo.

15. Ada za Usajili wa Alama ya Biashara au Huduma ni zipi?

- Ada ya Maombi Shs. 50,000/=
- Ada ya Kutangaza Maombi ya Alama Shs. 15,000/=
- Ada ya Usajili wa Alama Shs. 60,000/=
- Ada ya kutunza Alama (Maintenance Fee) Shs. 5,000/=

- Ada ya kuhuisha Alama Ths. 30,000/=

B. USAJILI WA HATAZA

1. Nini maana ya HATAZA?

HATAZA ni hati inayotolewa na Serikali kwa mvumbuzi kutokana na uvumbuzi alioufanya wa kitu au namna ya kuunda kitu unaolenga kutatua tatizo au kutoa jawabu/ufumbuzi mahsusi katika nyanja ya teknolojia husika.

Ili uvumbuzi upatiwe Hataza unatakiwa uwe mpya, uoneshe njia ya uvumbuzi na pia uweze kutumika katika eneo husika (new, inventive step and industrial applicability).

2. Je ni namna gani ninaweza Kusajili HATAZA?

HATAZA husajiliwa kupitia mfumo wa ORS

3. Ni vitu gani ambavyo vitaniwezesha kumiliki HATAZA?

Ill kupata umiliki wa Hataza aandae vitu vifuatavyo:-

(a). Jina la Uvumbuzi.

(b). Maelezo ya kina ya uvumbuzi katika nyanja husika (Patent Document).

(c). Maelezo yakidhi uelewa kwa mtaalam wa nyanja husika kuhusu teknologia iliyovumbuliwa na namna inavyoweza kutumika.

(d). Vielelezo kwa njia ya michoro maalum (Technical drawings).

4. Aina gani ya Uvumbuzi unalindwa kisheria?

(a). uvumbuzi uwe mpya au teknolojia mpya kwenye nyanja husika(novelty).

(b). Uwe na kigezo cha uvumbuzi kwenye nyanja husika (inventive step).

(c). Usiwe ni viumbe hai (mimea au Wanyama), usiwe ni nadharia za hisabati na za kisayansi, ugunduzi au mbinu za tiba.

(d). Ukidhi tathmini ya matumizi halisi (industrial applicability).

5. Je ni gharama kiasi gani inatumika kusajili HATAZA?

- Ada ya maombi ya Hataza ni Shilingi 12,000/= na ada ya ulinzi/ usajili Shilingi 10,000/=.
- Ada ya maombi ya Uvumbuzi Mdogo (Utility Certificate) ni Shilingi 10,000/= na ada ya ulinzi/usajili Shilingi 8,000/=.

6. Maombi ya hataza hushughulikiwa kwa muda gani?

Kuanzia kuwasilisha maombi ya Hataza mpaka kutolewa cheti ni *Siku 120 ikijumuisha siku za kutangazwa katika Jarida la Hataza.*

7. Je kuna malipo ya kila baada ya muda wa kumiliki HATAZA?

(a). Hataza (Patent) hulipiwa Shilingi 4000/= kwa mwaka wa kwanza na malipo haya ni ya kila mwaka kwa kuongezeka mpaka itakapoisha muda wake wa miaka ishirini.

(b). Hataza ndogo (Utility Certificate) hulipiwa Shilingi 3000/= kwa mwaka wa kwanza na Shilingi 1,000/= kila mwaka mpaka itakapoisha muda wa ulinzi wa miaka saba.

8. Je Hataza hudumu kwa muda gani?

Hataza hudumu kwa miaka ishirini (20) toka tarehe ya ulinzi kama ifuatavyo:-

Miaka kumi ya kwanza na kuhuishwa kwa miaka mitano mitano kwa kuwasilisha fomu na kulipia ada ya kuhuisha Hataza.

9. Ni nini natakiwa kufanya pindi Hataza yangu inapokwisha muda wake?

Hataza inapokwisha muda wake inakuwa huru (Public Domain) kutumika na mtu yeyote kwa ajili ya biashara ama vinginevyo

10. Ni namna gani naweza kupata taarifa za HATAZA ambayo imeshasajiliwa?

Taarifa za Hataza zinapatikana kwa kuwasilisha maombi kwa njia ya mtandao (ORS) sehemu ya "information services" na kuweza taarifa zinazoombwa pamoja na kulipia ada husika.

11. Kuna Tofauti gani kati ya HATAZA na ALAMA YA BIASHARA na HUDUMA?

HATAZA ni ulinzi unaotolewa kutokana na uvumbuzi, ALAMA YA BIASHARA ni alama ya kipekee ambayo imebuniwa na mwombaji wa alama hiyo kwa madhumuni ya kutofautisha kati ya bidhaa anazozitengeneza au huduma anayoitoa na bidhaa au huduma za watu wengine wanaotengeneza bidhaa kama zake au wanaotoa huduma kama yake.

12. Ni masuala yapi ya kuzingatia kabla na wakati wa kusajili Hataza?

(a). Maombi ya Hataza yawasilishwe kabla ya kuchapisha, kutoa muhadhara, Kufanya maonesho kuingia au kusaini mikataba ya matumizi ya uvumbuzi (Non disclosure of invention).

(b). Tambua eneo au maeneo ya ushindani wa uvumbuzi au teknolojia husika (commercial value or competitive advantage of patent exploitation).

(c) Maombi ya Hataza yanaweza kulindwa kupitia mfumo wa ulinzi wa Hataza kikanda na kimataifa (ARIPO na WIPO PCT Routes).

(d). Nyanja ya uvumbuzi inaweza kutumiwa vibaya hususan maangamizi ya ustawi wa jamii [silaha za kibaiolojia mfano kimeta (anthrax) katika vifurushi na barua].

4. Tembelea mfumo wa usajili kupitia https://ors, brela.go.tz au kupitia tovuti ya BRELA www.brela.go.tz na bofya LIMITED COMPANY ONLINE REGISTRATION.

SEHEMU YA NNE
MASWALI NA MAJIBU KUHUSU HUDUMA YA LESENI

A. LESENI ZA BIASHARA

1. Je kwa sasa BRELA ndio wanaotoa Leseni zote za biashara nchi nzima?

Hapana. Leseni zinazotolewa na BRELA ni zile za Kundi A tu ambazo zilikuwa zinatolewa na Wizara ya Viwanda na Biashara. Leseni za Kundi B ambazo zinatolewa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa bado zinaendelea kutolewa na Halmashauri.

2. Je wafanyabiashara ambao wanadaiwa Leseni za nyuma zilizotolewa nje ya mfumo kwa njia ya mtandao wanalipaje madeni hayo ndani ya mfumo?

Madeni wanayodaiwa wateja kwa ajili ya Leseni za kipindi kilichopita yanalipwa kwa mifumo ya awali iliyokuwa inatumika kabla ya kuanza kutumika kwa mfumo wa utoaji wa Leseni za biashara kwa njia ya mtandao.

3. Kwa mtu ambae ana leseni zilizopatikana nje ya mfumo anapotaka ku huisha leseni yake atatakiwa kuleta upya nyaraka zote alizokuwa ameleta awali?

Ndiyo:

kwa kuwa mfumo huu ndiyo utakuwa na kanzi data (data base) ya taarifa zote za Leseni za Biashara, mwombaji atatakiwa kuwasilisha nyaraka zote wakati wa kuomba Leseni katika mfumo.

4. Je naweza kutumia leseni moja hiyo hiyo kwenye maduka yangu mawili ambayo yako kwenye mtaa mmoja?

Hapana. Sheria ya Leseni za Biashara Sura 208 inataka kila eneo la biashara liwe na Leseni yake ya biashara. Hivyo, si sahihi kisheria maeneo mawili kutumia Leseni moja ya Biashara hata kama maeneo hayo yapo jatika mtaa mmoja.

5. **Ninapaswa kufanya nini ninaposimama kufanya biashara?**

   Unapofunga au Kusimamisha Biashara, unatakiwa kuwasilisha taarifa kwenye Mamlaka za Utoaji wa Leseni za Biashara (BRELA na Halmashauri) kuhusu ufungaji biashara.

6. **Je naweza kulipia leseni ya biashara kwa miaka kadhaa mfululizo?**
   Ndio. Unaweza kulipia Leseni ya Biashara kwa mfululizo kwa muda usiozidi miaka mitatu.

7. **Je Leseni zote za biashara sasa zinatolewa kwa njia ya Mtandao?**
   Hapana. sio leseni zote zinatolewa kwa njia ya Mtandao. Utoaji wa Leseni za Biashara kwa njia ya mtandao kwa sasa unafanyika kwa Leseni za Kundi 'A' ambazo ni Leseni zenye sura ya Kitaifa na Kimataifa,

8. **Kuna tofauti gani kati ya Leseni zinazotolewa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na zile zinazotolewa na BRELA?**

   Leseni za Kundi "A" zinazotolewa na BRELA ni kwa ajili ya Biashara zenye sura ya Kitaifa au Kimataifa au zinazoongozwa na Sera maalumu..

   Leseni za Kundi "B" zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri) nikwa ajili ya biashara zisizo na sura ya Kitaifa na Kimataifa au zisiozo ongozwa na Sera maalumu..

9. **Ni vigezo gani vya kuzingatiwa kwa Kampuni inapoomba Leseni ya Biashara.**
   Kampuni inapoomba Leseni ya Biashara hutakiwa kuwasilisha nyaraka zifuatazo:-
   a. Hati ya Usajili wa Kampuni
   b. Katiba ya kampuni inayoonesha majina Majina ya wamiliki wa Kampuni, Hisa wanazomiliki na Saini zao.
   c. Endapo wenye hisa wote wa kampuni au wamiliki wa biashara

wapo nje ya Nchi, Hati ya Uwakilishi iambatishwe;

d. Utambulisho wa Mkataba wa pango uliokamilika au Hati ya Umiliki wa jina la Biashara au Kampuni inayoomba Leseni kuonyesha eneo la kufanyia biashara;
e. Hati ya mlipa Kodi TIN nambaya Kampuni au Jina la Biashara;
f. Vitambulisho vya wenye hisa katika Kampuni au Wabia wa Biashara kama Hati ya kusafiria (Pasipoti), Kitambulisho cha Taifa, Kitambulisho cha kupigia kura na cheti cha kuzaliwa (kwa raia wa Tanzania); na Kibali cha kuishi nchini daraja ya "A" kwa wenye hisa wasio Watanzania.
g. Kibali kutoka kwenye mamlaka ya udhibiti (Wizara, Mamlaka, Idara, Taasisi au Wakala za Serikali) kuruhusu kufanyika kwa biashara husika.

10. Ni vitu gani vya kuwasilishwa mtu binafsi anaepotaka kuomba leseni

a) Kitambulisho cha Uraia wa mwombaji
b) Mkataba wa pango uliokamilika au Hati ya Umiliki kwa jina la mwombaji wa Leseni kuonyesha eneo la kufanyia biashara;
c) Kibali kutoka kwenye mamlaka ya udhibiti (Wizara, Mamlaka, Idara, Taasisi au Wakala za Serikali) kuruhusu kufanyika kwa biashara husika.

11. Ni vigezo gani vya kuzingatia kwa Kampuni ya Kigeni kuomba leseni?

Kampuni ya kigeni inayoomba Leseni ya Biashara hutakiwa kuwasilisha nyaraka zifuatazo:-

(a) Hati ya kuandikisha Kampuni (Certificate of Compliance)
(b) Endapo wenye hisa wote wa kampuni au wamiliki wa biashara wapo nje ya nchi, Hati ya Uwakilishi iambatishwe;
(c) Mkataba wa pango uliokamilika au Hati ya Umiliki kwa jina la Biashara au Kampuni inayoomba leseni kuonyesha eneo la kufanyia biashara;

(d) Hati ya utambulisho wa mlipa Kodi (TIN) ya Kampuni au Jina la Biashara.

(e) Vitambulisho vya wenye hisa katika Kampuni au Wabia wa Biashara kama Hati ya kusafiria (Pasipoti), Kitambulisho cha Taifa, Kitambulisho cha kupigia kura na cheti cha kuzaliwa (kwa raia wa Tanzania); na Kibali cha kuishi nchini daraja ya "A" kwa wenye hisa wasio Watanzania.

(g) Kibali kutoka kwenye mamlaka ya udhibiti (Wizara, Mamlaka, Idara, Taasisi au Wakala za Serikali) kuruhusu kufanyika kwa biashara husika.

12. Je, tunawezaje kupata msaada wa maelezo kutoka kwa Maafisa wanaoshughulikia Maombi ya Leseni za Biashara

BRELA ina namba maalumu ya huduma kwa mteja ambapo Mwombaji wa huduma anapokutana na changamoto zinazohitaji msaada wa kimaelezo kutoka kwa Maafisa wa Idara na Vitengo tofauti. Namba hizo zipo katika tovuti ya BRELA inayopatikana kwa anwani ifuatayo www.brela.go.tz. Pia, katika mfumo wa National Business Portal kuna namba ya simu ya kupiga kwa ajili ya kutoa msaada unaohitajika.

13. Namna gani mwombaji wa Leseni hulipa ada za Leseni za Biashara

Ada ya Leseni ya Biashara inalipwa baada ya mwombaji wa Leseni kuwasilisha nyaraka za kuomba leseni na kupitiwa na kuidhinishwa na Maafisa Leseni. Ada hizo zinalipwa kwa kutumia mfumo wa Kielektroniki wa malipo ya Serikali ambapo Mwombaji hupewa hati ya malipo (Invoice) yenye "Control Number". Baada ya kupata hati ya malipo, mwombaji anaweza kufanya malipo kwa njia zifuatazo:-

i. Kulipa Benki moja kwa moja kutegemea jina la Akaunti na Jina la Benki iliyoelekezwa katika hati ya malipo; au

ii. Kulipa kwa njia ya simu za mkononi (Mobile Money) ambapo mlipaji atachagua kulipa malipo ya Serikali, kuingiza namba ya malipo (Control Namba) na kulipa kiasi kilichoainishwa kwenye

hati ya malipo.

14. Adhabu ya kuchelewa kuhuisha Leseni ya Biashara ni kiasi gani?

Sheria ya Leseni za Biashara imetoa wigo wa siku ishirini na moja (21) kwa mwenye leseni kuhuisha leseni yake baada ya tarehe ya mwisho wa matumizi ya leseni husika. Zikizidi siku hizo, mwombaji hutakiwa kulipa adhabu ya kuchelewa ambayo ni asilimia ishirini na tano (25%) ya ada inayotakiwa kulipwa pamoja na ada ya wakati husika. Adhabu hiyo huongezeka kila baada ya siku thelathini (30) ikiwa mwenye leseni anaendelea kuitumia bila kuihuisha. Ongezeka hilo ni la asilimia mbili (2%) kila siku 30 zinapotimia.

15. Ni utaratibu gani unafuatwa kwa mteja kuomba leseni ya biashara katika mtandao kupitia mfumo wa "Tanzania National Business Portal"

Ili muombaji aweze kufanya maombi ya Leseni za Biashara katika mfumo hutakiwa kufuata hatua zifuatazo:-

i. Kujaza taarifa zake katika mfumo;
ii. Kujaza taarifa za biashara (Kampuni, jina la biashara au Binafsi);
iii. Kupakia nyaraka kama zilivyoainishwa katika mfumo na katika Sheria ya Leseni za Biashara;
iv. Kulipa ada ya Leseni kwa kutegemea aina ya biashara anayofanya;
v. Kupakua Leseni ya Biashara kupitia akaunti yake aliyoisajili.

16. Muda gani unatumika kwa mwombaji wa leseni kupata Leseni ya biashara

Kwa mwombaji ambaye amekamilisha taratibu na nyaraka zote zinazohitajika, Leseni inatolewa ndani ya dakika kadhaa baada ya kulipiwa ada na mwombaji kuthibitisha kuwa amefanya malipo husika.

B. LESENI ZA VIWANDA

1. Ili kupata Leseni ya Kiwanda/ Cheti Cha Usajili wa Kiwanda Kidogo ni vitu gani vinahitajika?

Jibu: Muomba Leseni ya Kiwanda/Cheti cha Usajili anapaswa kufanya na kuwasilisha kwa Msajili wa Viwanda kwa njia ya matandao nyaraka zifuatazo;

i. Kujaza fomu ya maombi na kuwasilisha
ii. Mchanganuo wa Mradi (Business Plan)
iii. Uthibitisho wa mahali Kilipo Kiwanda ambao ni Hati (Tittle Deed), Mkataba wa Pango (Lease Agreement) au Barua kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa (Local Government Authorities) husika.

2. Je kuna gharama yeyote ya kusajili Kiwanda/ Kupata Leseni ya Kiwanda?

Jibu: Ndiyo, kuna gharama ambazoanapaswa kulipa.

Gharama hizo hutofautiana baina ya Kiwanda kimoja na kingine kutegemea na Kiwango cha uwekezaji wa Kiwanda husika.

NA.	GHARAMA YA MRADI / UWEKEZAJI	ADA(TSH)
1.	Hauzidi Tsh 5,000,000	10,000
2.	Zaidi ya Tsh 5,000,000 lakini hauzidi 10,000,000	50,000
3.	Zaidi ya Tsh 10,000,000 lakini hauzidi 50,000,000	100, 000
4.	Zaidi ya Tsh 50,000,000 lakini hauzidi 100,000,000	500,000
5.	Zaidi ya Tsh 100,000,000	800,000

3. Leseni ya Kiwanda hudumu kwa muda gani?

Jibu: Muda wa kudumu Leseni hutegemea aina ya Leseni husika; Leseni ya Kiwanda ya Muda (Temporary Industrial Licence) hudumu kwa kipindi cha miaka mitatu, Leseni ya Kiwanda ya kudumu (Industrial Licence) haina ukomo wa muda na kwa upande wa Cheti cha Usajili (Certificate of Registration) ambacho hutolewa kwa Kiwanda Kidogo, hakina ukomo wa muda mpaka pale ambapo mtaji wa Kiwanda husika utaongezeka na kuwa na sifa ya kupewa Leseni ya Kiwanda.

4. Nini faida ya kusajili Kiwanda changu ama kuwa na Leseni ya Kiwanda?

Jibu: Kusajili Kiwanda kuna faida zifuatazo:-

Kwa mwenye Kiwanda:-

i. Kutekeleza matakwa ya Sheria ya Taifa ya Usajili na Leseni za Viwanda.
ii. Kurasimisha biashara
iii. Punguzo la Kiwango cha ushuru wa forodha (Import Duty) wakati wa uingizaji malighafi (Raw Materials) hapa nchini kwaajili ya Kiwanda husika.
iv. Kurahisisha upatikanaji wa vibali mbalimbali kama vile Leseni za biashara ambapo Leseni ya Kiwanda ni moja ya kiambatanisho muhimu katika upatikanaji wa Leseni ya Biashara.

Kwa Taifa

i. Makusanyo kwa Serikali yanayotokana na ada za usajili na utoaji wa Leseni hizo.
ii. Kupata taarifa na takwimu sahihi ya Viwanda pamoja na bidhaa zinazozalishwa ili kusaidia Serikali katika kuweka mipango na Sera madhubuti kwa maendeleo ya Sekta ya Viwanda na Taifa kwa ujumla.

5. Ni yapi madhara ya kutosajili Kiwanda/ adhabu kwa Kiwanda kisichokuwa na Leseni?

Jibu: Kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (2) cha Sheria ya Taifa ya Usajili na Utoaji wa Leseni za Viwanda, Sura ya 46 ya 1967 pamoja na marejeo yake ya mwaka 2002 (The National Industries (Licensing & Registration) Act. No 10 of 1967 Cap 46 RE 2002) ni kosa Kuanzisha ama kuendesha Kiwanda pasipo kuwa na Leseni ya Kiwanda ama Cheti cha Usajili wa Kiwanda kidogo.

6. Kuna tofauti gani kati ya Leseni za Viwanda na Leseni zinazotolewa na Halmashauri?

Jibu: Leseni hizi mbili zinatolewa kwa mujibu wa Sheria mbili tofauti, Leseni ya Kiwanda hutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Taifa ya Usajili na Utoaji wa Leseni za Viwanda, Sura ya 46 ya 1967 pamoja na marejeo yake ya mwaka 2002 (The National Industries (Licensing & Registration) Act. No 10 of 1967 Cap 46 RE 2002).ni kosa kuanzisha ama kuendesha Kiwanda pasipo kuwa na Leseni ya kiwanda ama cheti cha usajili wa kiwanda kidogo.

7. Ni mambo gani ambayo mmiliki wa Kiwanda kilichosajiliwa anapaswa kuzingatia baada ya kupata Leseni ya Kiwanda ama Cheti cha Usajili wa Kiwanda kidogo?

Jibu: Baada ya kusajili na kupata Leseni ya Kiwanda ama Cheti cha Usajili wa Kiwanda kidogo, mambo yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa:-

i. Kuwaslilisha kwa Msajili wa Viwanda taarifa ya maendeleo ya Kiwanda kila mwaka (Annual Progress Report)
ii. Kuwasilisha kwa Msajili wa Viwanda taarifa za Mabadiliko ya Taarifa za Kiwanda kama vile kuhamisha Kiwanda kutoka eneo moja kwenda lingine, kuongeza Tawi katika eneo lingine, kubadili umiliki wa Kiwanda n.k.
iii. Kuwasilisha Kwa Msajili wa Viwanda taarifa za Kuongeza bidhaa ambayo haikutajwa kwenye Cheti/Leseni husika.

iv. Kuwasilisha Kwa Msajili wa Viwanda taarifa za Kufunga Kiwanda ama kusimama uzalishaji.